

RITA, BODI YA MIKOPO WASAINI HATI YA MAKUBALIANO

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HELSEB) wamesaini hati ya makubaliano ili kurasimisha ushirikiano wa taasisi hizo mbili za Serikali kwa ajili ya kuwawezesha Waombaji wa Mikopo kupata huduma Bora na kwa wakati.

Tukio hilo limefanyika hii leo Jijini Dar es salaam ambapo hati hizo zimesainiwa na Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu/ Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA Bi. Emmy Hudson na Mkurugenzi Mtendaji wa HELSEB Dr. Abdulrazak Badru.

Katika Makubaliano hayo mambo muhimu yaliyobainishwa ni pamoja na, Wanafunzi wote wanaoomba mikopo ya Masomo HELSEB ni lazima waambatanishe Cheti cha Kuzaliwa na cheti cha kifo cha Mzazi kilichohakikiwa na RITA pamoja na kupeana uzoefu na mbinu mbalimbali katika masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEHAMA na kubadilishana taarifa za waliohakikiwa kwa kupitia mfumo wa kielektroniki.

Akiongea katika hafla hiyo, Dr. Badru amesema kwamba RITA na HELSEB zimekuwa zikifanya kazi kwa pamoja katika kuhakikisha kwamba wanafunzi walio na vigezo stahiki tu ndio wanaopatiwa mikopo ikiwemo uhakiki wa nyaraka hizo muhimu na kwamba uhusiano uliopo unaendelea kuwa bora kila mwaka kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA, Pia aliongeza kuwa tayari Serikali imeahidi kutenga Shilingi Bilioni 500 kwa ajili ya mikopo kwa mwaka ujao wa fedha na huu ukiwa uthibitisho tosha wa jinsi serikali inavyowajali wananchi wake.

“Naomba kusisitiza kwa wanafunzi wote wanaotegemea kuomba mikopo ya elimu ya juu kuanza sasa hivi kuandaa taarifa zao muhimu ikiwa ni pamoja na kuhakiki vyeti vya kuzaliwa na vifo kwa wale ambao wamefiwa na wazazi wao, wafanye hivi mapema kwani tunategemea kufungua dirisha la kupokea Maombi ya mikopo litafunguliwa tarehe 25 June 2021”. Alisema Dr. Badru.

Kwa upande wake Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu Bi. Emmy Hudson amesema kwamba tayari muongozo wa uhakiki umeshatolewa na zoezi la uhakiki kwa njia ya kielektroniki linaendelea na mpaka sasa tayari maombi 13938 Yamepokelewa na kati ya hayo vizazi 7434 na vifo 449 Yamejibiwa kikamilifu, hivyo nawaomba wazazi, walezi pamoja na wanafunzi kuhakikisha nyaraka hizo zinahakikiwa mapema ili dirisha la Bodi ya Mikopo litakapofunguliwa wawe wamekamilika.

“ Hapa leo tunachokifanya ni kuimarisha nguvu ya pamoja kama Taasisi za umma tumeona kuna haja ya kufanya kazi kwa pamoja na hili tumekuwa tukifanya tangu zamani kwa njia ya makaratasi isipokuwa kwa miaka mitatu hii mfumo umebadiriwa na sasa Uhakiki wote unafanyika kielektroniki kwa njia ya Mtandao kupitia mfumo wa E HUDUMA unaopatikana katika Tovuti ya Wakala www.rita.go.tz hivyo wanafunzi kuhakikisha wanaambatisha nakala zinazosomeka vizuri hasa namba ya ingizo (entry number) zikiwa katika mfumo wa pdf”. Alisema Bi. Hudson.